TANGAZO LA SERIKALI NA. 907 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

SHERIA NDOGO YA HIFADHI YA MAZINGIRA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MLIMBA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itaijulikana kama Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba.

Tafasiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo:

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"eneo la hifadhi" maana yake ni maeneo ya milima, maeneo ya vyanzo vya maji, hifadhi ya misitu, miteremko na maeneo mengine ambayo yatatangazwa na Halmashauri kuwa ni maeneo ya hifadhi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba;

"hifadhi ya mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi; mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji vinavyozingatia masharti na

maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria ya Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"kiwanda" maana yake ni jengo au eneo ambapo vitu vinatengenezwa;

"kuvuna misitu" inajumuisha kufyeka, kukata au kung'oa misitu au visiki;

"maeneo ya malisho" maana yake ni maeneo yaliyotemgwa kwa ajili ya malisho ya mifugo, pamoja na sehemu zote ambazo zimetengwa na Halmashauri kwa ajili ya malisho;

Sura ya 191 "maji" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 191 "maji taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

Sura ya 323 "mazao ya misitu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Misitu;

Sura ya 191 "mazingira" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mfugaji" maana yake ni mtu yeyote anaejishughulisha na ufugaji wa mifugo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

Sura ya 323 "misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 ya miti, uoto wa asili au iliyopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota upya ambayo itajumuisha aina yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangazwa chini ya Sheria ya Misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

Sura ya 191 "taka" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"taka ngumu" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika

Sheria ya Usimamizi Mazingira;

"udongo" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

Wajibu wa Halmashauri

4.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya shughuli za malisho ndani ya eneo la Halmashauri.

(2) Halmashauri itatenga njia maalum ya kupitisha mifugo kwenda na kurudi malishoni au minadani.

(3) Halmashauri itafanya Sensa ya mifugo na kutoa kadi za mifugo na elimu ya ufugaji bora kwa jamii.

Wajibu wa mfugaji

5. Kila mfugaji chini ya Sheria Ndogo hii atatakiwa-

(a) kufuga na kulisha mifugo katika maeneo ya malisho yaliyopangwa na Halmashauri;
(b) kupitisha mifugo yake katika njia zilizopangwa na kutengwa na Halmashauri;
(c) kuwa na kadi ya mifugo itakayoonesha idadi na aina ya mifugo aliyonayo;
(d) akupeleka mifugo katika josho kama atakavyoagizwa na Halmashauri;
(e) kupeleka mifugo yake katika vituo vya chanjo kama itakavyoamriwa na Halmashauri, na atalipia chanjo hiyo kama atatakiwa kufanya hivyo;
(f) kuchangia gharama za ukarabati wa josho kama sehemu ya mchango wake, pale itakapobidi kufanya hivyo, na kwa gharama itakayopendekezwa na Halmashauri;
(g) kuchangia gharama za uboreshaji wa maeneo ya malisho yaliyotengwa na Halmashauri;
(h) kuweka alama kwenye mifugo yake na katika viungo vya mifugo vinavyopendekezwa ili kutoharibu zao la ngozi;
(i) kuhudhuria mafunzo ya ufugaji kama

atakavyohitajiwa na Halmashauri;

(j) kutokata miti kwa lengo la kufukuza mbung'o; na

(k) kusajili mifugo katika rejista ya Kijiji nakuogesha mifugo katika majosho kama ratiba itakavyopangwa.

Marufuku kwa mfugaji

6. Itakuwa marufuku kwa mfugaji yeyote-

(a) kuchunga, kulisha au kunywesha maji mifugo katika maeneo yote ambayo hayakutengwa kwa ajili hiyo;

(b) kusafirisha mifugo kwa kuiswaga barabarani zaidi ya kilometa thelathini;

(c) kusafirisha au kuhamisha mifugo kutoka eneo moja hadi lingine bila kibali kutoka Halmashauri;

(d) kuingiza mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali kitakachotolewa na Halmashauri;

(e) kuuza au kununua mifugo katika maeneo ambayo siyo mnada, soko au gulio la mifugo lililoidhinishwa na Halmashauri; na

(f) kupitisha mifugo katika maeneo ambayo hayakuidhinishwa na Halmashauri.

Kudhibiti mifugo inayozurura ovyo

7.-(1) Halmashauri itakamata mifugo itakayoonekana inazurura ovyo katika eneo la Halmashauri ambalo halijaruhusiwa kuchungia mifugo.

(2) Mfugo wowote utakaokamatwa mahali pasipostahili utalipiwa faini ya shilingi elfu ishirini kwa kila mfugo na baada ya kulipia gharama hizo mfugaji atarudishiwa mfugo wake.

(3) Endapo mfugo uliokamatwa hautachukuliwa na mmiliki ndani ya kipindi cha siku saba tangu kukamatwa, Halmashauri itakuwa na haki ya kuuza kwa mnada mfugo huo baada ya kupata idhini ya Mahakama, na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mfugo huo

baada ya kutoa faini inayodaiwa, gharama za kuhifadhi mfugo, gharama ya Mahakama na gharama ya mnada.

(4) Bila kuathiri aya ndogo ya (3), kabla ya kuuza mfugo huo kwa mnada, Halmashauri itamjulisha mmliki na umma juu ya kusudio hilo.

(5) Endapo kutatokea kufa kwa mifugo kutokana na sababu yoyote, Halmashauri haitawajibika na ulipaji wa gharama zozote isipokuwa kama vifo hivyo vitakuwa vimesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Ukaguzi wa mifugo

8.-(1) Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika boma au jengo lolote kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni Kwa dhumuni la kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakayemzuia Afisa Mwidhiniwa katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa.

Taratibu za ufugaji

9.-(1) Wafugaji wote watatakiwa kuzingatia masharti ya kufuga kama yalivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(2) Kila mfugaji atatakiwa kupeleka mifugo yake machinjioni au mahali huduma hiyo inapopatikana na itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchinja mifugo mahali pengine popote ambapo sio machinjio isipokuwa kwa kutoa taarifa kwa Afisa Mwidhiniwa na atalazimika kulipia gharama za machinjio kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

(3) Ni marufuku kwa mtu yeyote kununua, kuuza au kufanya biashara ya kubadilishana aina yoyote ya mifugo katika eneo lolote la Halmashauri isipokuwa kwenye minada au magulio yaliyotengwa kwa shughuli hiyo.

(4) Mfugaji atawajibika kumfungia mbwa wake wakati wote wa mchana na atamfungulia kuanzia saa nne

kamili usiku na kumfungia saa kumi na mbili kamili.

Taratibu za Kilimo

10.-(1) Mtu atakayetaka kuendesha shughuli za kilimo katika Halmashauri atatakiwa kuzingatia taratibu za kilimo kama zitakavyotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia Sheria husika za ardhi.

(2) Afisa mwidhiniwa anaweza kuingia katika shamba lolote kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni. kwa dhumuni la kukagua utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Marufuku

11.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kulima katika miteremko, au karibu na vyanzo vya maji au kandokando ya mito au mabwawa na maziwa au kufanya jambo lolote litakalo haribu hifadhi ya mazingira;

(b) kutumia ardhi kinyume na matumizi ya kilimo kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Halmashauri.;

(c) kusafisha shamba kwa ajili ya kilimo kwa njia ya kuchoma moto isipokuwa kwa kibali maalum kutoka Halmashauri; au

(d) kutupa mabaki ya vifungashio vya viuatilifu au kusafisha vipulizi au kumwaga mabaki ya viuatilifu katika chanzo cha maji au mto.

(2) Kibali kitakachotolewa chini ya Sheria Ndogo hii kitakuwa cha maandishi na kitaonesha jina la mwenye kibali, tarehe na eneo analotaka kuchoma moto.

(3) Muda unaotakiwa kuchoma moto chini ya Sheria Ndogo hii ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa nne kamili asubuhi.

(4) Ni wajibu wa Halmashauri kusimamia shughuli za kilimo na kuzuia kilimo cha kuhamahama na kuhimiza kilimo cha mzunguko.

Uhifadhi wa uoto wa asili

12. Ni wajibu wa wakazi wa eneo ambalo uoto wa

asili au mazingira ya eneo husika yameharibiwa, kuhakikisha kua wanalirudisha katika hali yake ya kawaida kwa kupanda miti ili kutoendelea kuharibu mazingira.

Uchimbaji mchanga na kokoto

13.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba mchanga au kifusi au kuchoma tofali katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri kama vile katika maeneo ya makazi ya watu, maeneo yaliyohifadhiwa, kando kando ya mito au ndani ya mto, bwawa au ziwa isipokuwa kwa ruhusa maalumu ya Halmashauri.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kujenga nyumba au jengo lolote au kufanya shughuli zozote za kiuchumi katika eneo la hifadhi.

Wajibu wa kulinda vyanzo vya maji

14.-(1) Halmashauri itawajibika kusimamia na kulinda vyanzo vya maji.

(2) Halmashauri itachukua hatua kali za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi.

(3) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri na jamii husika kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

(4) Ni marufuku kwa mtu yeyote kumiliki eneo la chanzo cha maji.

Kulinda eneo la Hifadhi

15.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kulima au kukata miti au kuchunga mifugo katika umbali wa mita 60 kutoka chanzo cha maji au kufanya jambo lolote linaloharibu kwa namna yoyote chanzo cha maji na hifadhi ya mazingira.

(2) Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya majivilivyo katika maeneo ya hifadhi kwa kuzingatia maelekezo ya Afisa Misitu.

Uchafuzi wa vyanzo vya maji

16.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuelekeza mabomba ya maji machafu kwenye mito, mabwawa, ziwa, visima, mifereji, chemchemi au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka kitu chochote chenye sumu ndani ya maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote hai.

Kuchoma au kusababisha moto

17.-(1) Mtu yeyote hataruhusiwa kuchoma au kusababisha moto katika misitu iliyoko eneo la Halmashauri.

(2) Ni wajibu wa kila mwananchi kuzima moto ambao utaonekana kuwaka katika eneo la Halmashauri wenye viashiria vya kuleta hatari.

(3) Kila mkazi wa eneo hilo atawajibika kushiriki katika zoezi la kuzima moto endapo atatakiwa kufanya hivyo na endapoatashindwa kushiriki katika zoezi la kuzima moto bila sababu ya msingi atakuwa ametenda kosa.

Kibali cha kuchoma moto

18. Mtu yeyote aliyepata kibali cha kuchoma moto atalazimika kutoa taarifa ya siku mbili kabla ya kuchoma moto kwa majirani walioko katika eneo analotaka kuchoma na ataweka njia za kuzuia moto kusambaa maeneo mengine.

Ukataji miti

19.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote-

(a) kukata miti kwa ajili ya matumizi ya aina yoyote bila kupata kibali kutoka Halmashauri; au

(b) kuvuna miti katika msitu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya viumbe hai maalum ambao ni rasilimali kwa Taifa.

(2) Watu wanaovuna miti kwa ajili ya kuchoma mkaa wanatakiwa kuwa na eneo maalumu lililoidhinishwa

na Halmashauri kwa ajili ya kuchoma mkaa.

Wajibu wa kupanda miti

20. Kila mkazi wa Halmashauri atawajibika:
(a) kupanda na kutunza miti katika eneo lake;
(b) kupanda na kutunza miti katika makazi yake; na
(c) kupanda na kutunza miti katika shamba au mashamba anayomiliki.

Wajibu wa Halmashauri ya Kijiji

21. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kila Kijiji-
(a) kitawajibika kutenga eneo la hifadhi ya Msitu wa asili kwa ajili ya matumizi ya baadaye;
(b) kinatunza miti yote inayopandwa katika eneo la Kijiji;
(c) kitasimamia kila Kaya kupanda miti katika maeneo yao kila Mwaka;
(d) kinapanda na kumiliki shamba la miti lenye ukubwa wa ekari mbili kila mwaka na kulitunza;
(e) kila Taasisii ndani ya Halmashauri itapaswa kupanda miti ya kukinga upepo kuzunguka majengo yake na kuwa na shamba lisilopungua miti hekta mbili;
(f) kinatunza na kuhifadhi miti na nyasi kwenye milima, makorongo na vyanzo vya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo;
(g) kitahakikisha kuwa kila anayeandaa shamba kwa ajili ya kilimo hatumii moto bila kibali na anapanda miti kwenye mipaka ya shamba lake kama kinga upepo;
(h) kitahakikisha kuwa kila Mwenyekiti wa Kitongoji, Mtendaji wa Kijiji, Mkuu wa Taasisi yoyote Wilayani ana msitu wa hifadhi ya miti ya kupandwa au ya asili kwa madhumuni ya kuhifadhi ardhi na mazingira;
(i) kitahakikisha kuwa maeneo yote ya vilima na yenye vipara ambayo yanamilikiwa na watu

binafsi au Serikali ya Kijiji yanapandwa miti.

Utupaji wa taka ngumu na laini

22.-(1) Ni wajibu wa Halmashauri kutenga eneo kwa ajili ya kutupa taka ngumu au laini na kusimamia kwa karibu usafi katika eneo lake.

(2) Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini, au kujisaidia katika kingo za mabwawa au kwenye vyanzo vya maji vilivyoko katika Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa viwanda, vituo vya mafuta na huduma za ujenzi

23.-(1) Mtu yeyote anayeendesha shughuli za karakana, mashine ya kusaga, kuranda mbao, kukamua maji ya matunda, kuchomelea vyuma au kuendesha shughuli yoyote inayozalisha uchafu ambao unaleta athari kwa binadamu na viumbe wengine hai katika maeneo ya makazi ya watu atatakiwa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo hii.

(2) Endapo mtu yeyote anataka kuendesha shughuli za kiwanda, kituo cha mafuta, kituo cha huduma mbalimbali za ujenzi atatakiwa kuzingatia tahadhari ya athari za mazingira.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya aya ya (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu mifugo

24. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa-

(a) ataingiza mfugo au mifugo katika eneo la Halmashauri bila kibali;

(b) atasafirisha mfugo au mifugo bila kuwa na kibali;

(c) atalisha mfugo au mifugo katika maeneo yasiyoruhusiwa;

(d) atavua samaki kwa kutumia sumu au nyavu zenye matundu madogo (kokoro).

Makosa yanayohusu kilimo

25. Mtu yeyote atakayekiuka masharti kuhusu kilimo yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii atakuwa

ametenda kosa.

Makosa yanayohusu hifadhi ya ardhi

26. Mtu yeyote atakayekiuka masharti kuhusu kuhifadhi ardhi yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu vyanzo vya maji

27.-(1) Mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote atakayeweka sumu ya aina yoyote ambayo inaathiri maisha ya binadamu na viumbe hai atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu mazao ya misitu

28. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa ikiwa-

(a) atachoma au kusababisha moto katika misitu bila kibali;
(b) atashindwa kushiriki katika kuzima moto;
(c) atavuna mazao ya misitu katika misitu iliyohifadhiwa na isiyohifadhiwa bila kibali;
(d) atachoma mkaa na kukata kuni bila kibali;
(e) atafyeka nyasi, kung'oa vichaka na kung'oa visiki kwenye misitu bila kibali;
(f) atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti, iliyohifadhiwa kama bustani ya miti, msitu ya asili au iliyopandwa kwa ajili ya hifadhi;
(g) atakata miti au kuchungia mifugo kwenye miti iliyopandwa kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo au kinga upepo;
(h) atabandua magome ya miti kwa ajili ya kutengeneza vilindo, mzinga na vitu vingine bila ya kuwa na kibali; na
(i) atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.

Makosa yanayohusu taka ngumu na laini

29. Mtu yeyote atakayetupa ovyo taka ngumu au laini katika maeneo yoyote yasiyoruhusiwa na Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa.

Makosa yanayohusu taka za majimaji

30. Mtu yeyote atakayetiririsha maji machafu yanayoleta madhara kwa binadamu na viumbe hai wengine atakuwa ametenda kosa.

Adhabu

31. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

32. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 32)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFILILILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. Mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …..… ya Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU
Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….
Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:
Jina: …………………………………..……………………
Saini……………………….…………………………..………
Wadhifa: ………………………………………………………
Tarehe……………………………………………………….

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Mlimba imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmshauri ya Wilaya ya Mlimba uliofanyika Tarehe 27 Mwezi Oktoba Mwaka 2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

ENG. STEPHANO B. KALIWA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

INNOCENT SIMON MWANGASA
*Mwenyekiti*

*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*